

**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kulia), akielekezwa jambo na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel wakati wa kikao na baadhi ya wakulima na wafugaji wanaofanya shughuli zao kwenye Ranchi ya Usangu iliyopo Wilaya ya Mbarali Mkoani Mbeya, pamoja na baadhi ya wawekezaji waliopatiwa vitalu katika ranchi hiyo. Waziri Ndaki amefanya ziara ya kikazi ya siku mbili mkoani humo ili kutambua changamoto zilizopo kwenye Ranchi ya Usangu na kuzitafutia ufumbuzi.** (Picha na Edward Kondela)

# Waliokaidi mkataba wa NARCO kikaangoni

**Na Edward Kondela**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki ametoa siku kumi kwa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kubaini na kuwanyang'anya maeneo, wawekezaji waliopatiwa vitalu katika ranchi za taifa ambao wamebadili matumizi ya ardhi kinyume na makubaliano ya mikataba yao.

Waziri Ndaki amebainisha hayo juzi wakati alipotembelea Ranchi ya Usangu iliyopo Wilaya ya Mbarali Mkoani Mbeya alipokuwa kwenye ziara ya kikazi ya siku mbili mkoani humo na kufanya mkutano wa hadhara na baadhi ya wawekezaji, wakulima na wafugaji, ambao wanafanya shughuli zao katika ranchi hiyo na kubaini kuwa baadhi ya wawekezaji waliopatiwa vitalu na NARCO kwa ajili ya kufuga na kulima malisho ya mifugo wamekuwa wakikodisha maeneo hayo kwa wakulima na wafugaji kinyume na mkataba.

"NARCO siku kumi nadhani zinawatosha kubaini watu wanaojiita wawekezaji, waliobadilisha matumizi ya ardhi ambayo siyo kufuga wala malisho wanyang'anywe maeneo kwa kuwa wameenda kinyume na utaratibu wa mkataba kati yao na NARCO, na mimi nitafuatilia nitapenda kupata taarifa mmepata wangapi na wangapi wamenyang'anywa kwa kuwa wameenda kinyume na utaratibu waliokubaliana" alisema Ndaki.

Waziri Ndaki amelazimika kutoa kauli hiyo baada ya kupata taarifa kutoka kwa baadhi ya wakulima na wafugaji wa Wilaya ya Mbarali kuwa wamekuwa wakikodishwa maeneo ya ranchi hiyo na wawekezaji kwa shilingi 20,000 kwa hekari moja kwa ajili ya kilimo na madebe kumi ya nafaka baada ya mavuno kwa kila hekari moja, huku wafugaji wakilipa takriban shilingi milioni mbili kwa hekari moja katika kipindi cha miezi minne kwa ajili ya kulisha mifugo yao kwenye maeneo ya wawekezaji ambao wamepatiwa vitalu na NARCO kwa mkataba wa kufuga au kulima malisho ya mifugo.

Alifafanua kuwa mkataba wa NARCO na wawekezaji kwa ajili ya kufugia mifugo na kulima malisho hauruhusu wawekezaji kukodisha eneo kwa mtu mwingine kwa ajili ya shughuli zozote kwa kuwa maeneo ya ranchi za taifa ni mali ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO).

Kuhusu deni la zaidi ya Shilingi Bilioni Sita ambalo NARCO inawadai wawekezaji waliopatiwa vitalu katika ranchi za taifa zilizopo kwenye maeneo mbalimbali nchini,Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki ameutaka uongozi wa NARCO kufikia Februari 15 mwaka 2021 saa saba mchana awe amepata taarifa ya wawekezaji waliolipa madeni yao pamoja na ambao bado hawajalipa, kabla ya kuchukuliwa kwa hatua zaidi.

"Wawekezaji wote ambao tunawadai hapa Usangu na kwenye ranchi zingine wote walipe pesa ya NARCO tulipokubaliana kwenye mkataba tulikubaliana mtalipa pesa, mlipe madeni yenu ifikapo tarehe 15 mwezi februari saa saba mchana muwe mmelipa madeni yenu tunataka NARCO ijiendeshe kibiashara,lakini sioni tukielekea kwenye kujiendesha kibiashara na moja ya matatizo yanayotufanya tusifike huko ni kulea watu wa namna hii," alifafanua Ndaki.

Aliongeza kuwa wale ambao hawatakuwa wamelipa hadi kufikia muda huo wanyang'anywe maeneo hayo ili wapatiwe watu wengine ambao wataweza kulipa kwa mujibu wa mkataba ili NARCO iweze kufikia malengo yake na kulalamika kuwa NARCO imechelewa kuchukua hatua kwa watu ambao wamekuwa na madeni ya siku nyingi.

Alisema kuwa wizara imefanya tathmini juu ya madeni hayo na kuagiza yalipwe katika viwango na tozo mpya zilizowekwa kwa sababu imejindhisha kwamba kwa gharama hizo NARCO itaweza kujiendesha na kuhudumia vizuri ranchi zake.

Kwa mujibu wa taarifa ya NARCO iliyotolewa na Kaimu Meneja Mkuu wa kampuni hiyo Masele Mipawa, maeneo ya vitalu katika ranchi za taifa yanayokodishwa kwa wawekezaji yamegawanywa katika viwango vitatu, ambapo kiwango cha chini ni Sh.3,500 kwa hekari moja kuanzia eneo lenye hekta 1 hadi 2000, kiwango cha kati ni Sh.5,500 kwa hekari moja kuanzia eneo lenye hekta kuanzia hekta 2001 hadi 5000 na kiwango cha juu ni Sh. 7,500 kwa hekari moja kuanzia eneo lenye hekta zaidi ya 5001.

MAJIRA – 19/01/2021 Pg. 16.

Scanned with CamScanner

# Mifugo 12,000 katika vijiji sita kufaidi josho

Na Cheji Bakari, Kilindi

TAKRIBANI mifugo 12,000 katika vijiji sita vya kata za Songe na Masagalu imetoka katika hatari ya kukumbwa na magonjwa ya mifugo baada ya serikali wilayani Kilindi kukamilisha ujenzi wa josho la mifugo lililokuwa limetelekezwa kwa zaidi ya miaka kumi.

Wakizungumza baada ya uzinduzi wa josho hilo lililojengwa katika kijiji cha Kwamba katika Kata ya Songe, wananchi wa vijiji hivyo ambao wengi ni jamii wafugaji walishukuru wakisema kukamilika kwa ujenzi wa josho hilo kutawondolea kero.

Mmoja wa wafugaji wa jamii ya Kimaasai, Lengisho Shami, alisema wamefarijika kukamilika kwa josho hilo kwani asilimia kubwa ya mifugo ilikuwa ikipoteza maisha kutokana na magonjwa mbalimbali ya mifugo.

Shami alisema kukosa huduma ya josho ilikuwa tishio kwa mifugo yao kutokana na magonjwa.

Issa Nurdin alisema kufunguliwa kwa josho hilo ni fursa kwao kuendeleza sekta ya mifugo kwa kuwa ni moja ya vyanzo vyao vikuu vya mapato.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kwamba lilipo josho hilo, Abdi Makinda, alisema mradi huo ulianzishwa baada ya serikali kusikia kilio chao, lakini kwa zaidi ya miaka kumi ulikuwa umetelekezwa.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kunavinufaisha vijiji sita vilivyopo katika kata za Songe na Masagalu na kwamba, takriban mifugo 12,000 watapata huduma katika josho hilo mara tatu kwa wiki.

Kwa mujibu wa Makinda, vijiji vinavyonufaika na mradi huo ni Kwamba, Miluzi, Kigunga, Misheni, Mheza na Sambu.

Kabla ya kukamilika kwa josho hilo, wafugaji hao walikuwa wakilazimika kufuata huduma hizo Songe umbali uliokuwa na athari kwa mifugo yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, Gracian Makota, alisema mradi huo umegharimu Sh milioni 37.4.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi imechangia Sh milioni 1.16 huku nguvu za wananchi zikiwa ni Sh 300,000.

Scanned with CamScanner

# Mbunge alalamikia uingizaji wa mifugo Namtumbo

**Na Yeremias Ngerangera, Namtumbo**

MBUNGE wa Jimbo la Namtumbo mkoani Ruvuma, Vitta Kawawa kupitia kikao cha maendeleo ya mkoa kilichofanyika hivi karibuni amelalamikia uingizaji wa mifugo katika jimbo hilo.

Katika kikao hicho, Kawawa aliwaambia wajumbe kuwa uingizaji wa mifugo katika Wilaya ya Namtumbo kuna dalili za migogoro kuanza kujitokeza kati ya wakulima na wafugaji waliopo, lakini wimbi kubwa la wafugaji linaloendelea kuingia litaongeza migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Kawawa alidai Namtumbo, ilitenga maeneo ya kilimo kwa ajili ya wakulima hifadhi ya misitu kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi pamoja na hifadhi za wanyama pori zilizopo chini ya Jumuiya ya Hifadhi za wanyama pori za Kimbanda, Kisungule na Mbarang'andu.

Akizungumzia hatua hiyo Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Ruvuma, Oddo Mwisho alisema kila wilaya ihakikishe inakuwa na kikao cha kuangalia namna bora ya kutatua migogoro kati ya wafugaji na wakulima, hifadhi za wanyamapori na wakulima wanaozunguka kwenye hifadhi na wafugaji wanaofanyia shughuli zao kkatika hifadhi kinyume na utaratibu.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Madaba, Joseph Mhagama alimwomba Mwenyekiti kuwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya hifadhi ya misitu na maeneo ya mapito ya wanyama (USHOROBA) katika wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma, yaheshimiwe kwa kuwa yanavamiwa na wananchi kwa nguvu na kuwatoa kwake pia kunahitajika nguvu.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme alisisitiza kuheshimu maeneo yalioyotengwa kwa ajili ya hifadhi ya misitu na mapito ya wanyama ambapo aliwataka wananchi waliovamia maeneo hayo kuondolewa.

Pia akiwataka wananchi wa Kitongoji cha Semeni Kijiji cha Lingusanguse wilayani Namtumbo, kutohusika katika kuondolewa huko kwa kuwa licha ya kitongoji hicho kwepo katika eneo lililotengwa la mapito ya wanyama, tatizo hilo linashughulikiwa ngazi ya kitaifa.

Scanned with CamScanner

a
ni
o

a
a
a

a
a
ki
o
gi
ie
ta

# Mvuvi afa maji baharini

MAJIRA - 19/01/2021 UK. 2

**Na Said Hauni, Lindi**

MVUVI na mkazi wa Kijiji na Kata ya Nachunyu,Tarafa ya Sudi Halmashauri ya Mtama mkoani Lindi,Hafidhi Ally (20) amefariki alipokuwa akivua aina mbalimbali ya samaki kwenye Bahari ya Hindi.

Taarifa kutoka tarafa hiyo na kuthibitishwa na Jeshi la Polisi mkoani humo zilieleza kwamba, Hafidhi Ally alipatwa na umauti huo Januari 14 mwaka huu.

Wakizungumza na gazeti hili baadhi ya ndugu na mashuhuda wa mwili wa mvuvi huyo,Juma Yusufu,Idrisa Ally,Maulidi Daudi na Mwanabibi Hemedi walisema siku hiyo ya Januari 14,mwaka huu asubuhi,Ally aliondoka nyumbani kwake kwenda Baharini kuwa samaki,lakini hakuweza kurejea nyumbani. Pia walieleza kwamba kitendo cha kutorejea nyumbani kiliwapa hofu ndipo zoezi la kumsaka lilipoanza na kufanikiwa kuupata mwili wake Januari 17, mwaka huu,ukiwa ndani ya mtumbwi aliokuwa akiutumia kuvulia samaki. "Mwili wa marehemu Ally tumefanikiwa kuupata Januari 17 mwaka huu ukiwa ndani ya mtumbwi ukielea baharini walieleza mashuhuda hao," alisema.

Aidha, walieleza kwamba licha ya kuukuta mwili huo ukiwa ndani ya mtumbwi huo pia walifanikiwa kukuta samaki aina ya Changu na Chewa wasiopungua kumi aliokuwa amefanikiwa kuwavua kwa siku hiyo. "Tunaweza kusema ni ahadi tu imemfikia,kwani tungemkuta anaelea majini na mtumbwi upo peke yake,tungesema labda dhoruba ya upepo,lakini tumemkuta ndani ya chombo alichokuwa anakitumia," alisema Yusufu.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Foka Dinya alithibitisha kutokea kwa kifo cha mvuvi huyo, huku akitoa taadhari kwa wavuvi kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa utabiri wa hali ya hewa nchini kutokana na upepo mkali unaoendelea kuvuma kwenye Bahari ya Hindi.

Scanned with CamScanner

MAJIRA - 18/01/2021 - uk 3.

# Afisa mifugo Igunga asimamishwa kazi

**Na Allan Vicent, Tabora**

KAIMU Mkurugenzi wa Halmashauri Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, Pascrates Kweyamba amemsimamisha kazi kwa muda usiojulikana Ofisa Mifugo Msaidizi, Mussa Mrisho Kato wa Kata ya Lugubu kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake juzi alisema, hatua ya kumsimamisha kazi imetokana na taarifa aliyoletewa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilaya hapa ya kumjulisha kuwa mtumishi huyo amefikishwa mahakama ya wilaya akituhumiwa kwa makosa manne ya kuomba na kupokea rushwa ya shilingi 500,000.

"Ofisi yangu ilipokea barua kutoka ofisi ya TAKUKURU ikinijulisha kuwa mtumishi huyo ambaye alikamatwa na taasisi hiyo akiomba na kupokea rushwa, hivyo nimeamua kumsimamisha kwa muda usiojulikana mpaka pale kesi yake ya msingi Na. 1/2020 itakapoisha mahakamani,"alisema.

Aidha, aliongeza kuwa mtumishi huyo licha ya kuonywa mara kwa mara kutokana na vitendo hivyo bado aliendelea na tabia hiyo.

Kwenyamba aliongeza kuwa, mtumishi huyo pia amekuwa si mwaminifu kwani fedha za ushuru wa mazao anazokusanya amekuwa akizitumia kinyume na utaratibu akitoa mfano wa sh.milioni 9 alizokusanya na kuzitumia na hadi sasa amerejesha sh.milioni 6 tu bado anadaiwa milioni 3.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi wilaya humo, Erick Sije alionya watumishi ambao wamekuwa vikwazo katika maeneo yao ya kazi kwa kulalamikiwa na wananchi kwa kula fedha zinazochangwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo na kuongeza kuwa ofisi yake haitamvumilia yeyote atakayebainika kwenda kinyume na sheria na kanuni za utumishi wa umma.

Aliagiza watendaji wote wa vijiji na kata kuhakikisha wanasoma taarifa za mapato na matumizi kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kutatua kero zinazowakabili wananchi.

"Watumishi lazima tubadilike ili kuendana na kasi ya Rais wetu Dkt.John Pombe Magufuli kwani amekuwa akisisitiza uadilifu kila mara katika utumishi wetu kwa wananchi,"alisema.

Ofisa huyo alipoulizwa juu ya kusimamishwa kazi alikiri kupokea barua tangu Desemba 23, 2020 na kusema kuwa atazingatia maelekezo hayo hadi kesi yake itakapoisha.

Scanned with CamScanner

# Mazao ya uvuvi yaingiza bilioni 4/-

Na Yohana Shida, Geita

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amesema ndani ya kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015 hadi 2020 serikali imefanikiwa kukusanya takribani Sh bilioni nne kutokana na biashara ya mazao ya uvuvi ikiwemo dagaa.

Mashimba alisema hayo wiki iliyopita akiwa wilayani Chato, mkoa wa Geita wakati akitoa taarifa ya maendeleo ya sekta hiyo nchini mbele ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk Hussein Mwinyi alipotembelea Soko la Kimataifa la Dagaa la Kasenda.

Alisema mapato hayo yanatokana na kukua kwa biashara ya samaki nje ya nchi, ambapo mwaka jana jumla ya tani 5,725 za mazao ya uvuvi yenye thamani ya Sh bilioni 7.5 yaliuzwa nje ya nchi na serikali ilipata mrabaha wa Sh bilioni 2.4, ikilinganishwa na tani 4,571 zilizouzwa mwaka 2019 zenye thamani ya Sh bilioni 6.7 na serikali kupata mrabaha wa Sh bilioni 1.7.

Alisema kupitia mapato ya halmashauri, serikali imefanikiwa kukusanya takribani Sh milioni 225 ndani ya kipindi ya miaka miwili iliyopita kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka jana.



Mashimba alisema mafanikio hayo yamechagizwa na juhudi za serikali kuboresha na kuongeza thamani ya mazao ya samaki na kuweka miundombinu rafiki katika sekta ya uvuvi kwa kujenga masoko rasmi yanayotumika kupokelea na kuhifadhi samaki yapatayo 16 ikiwamo masoko sita yaliyopo Kanda ya Ziwa Victoria na mawili Kanda ya Ziwa Tanganyika.

Waziri huyo alisema pia serikali imeendelea kujenga na kuboresha mialo ya kupokelea samaki, ambapo kwa Kanda ya Ziwa Victoria kuna mialo 26, Kanda wa Ziwa Tanganyika mialo minne na mialo mitatu Kanda ya Bahari ya Hindi.

"Kwa mkoa wa Geita kuna jumla ya mialo midogo 73 ya kupokelea samaki, kutokana na uwapo wa idadi kubwa ya eneo la uvuvi, huku wilaya ya Chato ndiyo inaongoza kwa kuwa na jumla ya wavuvi 8,259 na vyombo vya uvuvi 2,755."

"Uzalishaji wa samaki mkoani Geita umekua kwa kasi kutoka mwaka 2015 ambapo zilivunwa takribani tani 18,535 zenye thamani ya Sh bilioni 76.9 ikilinganishwa na tani 21,188 zizovunwa mwaka 2019 zikiwa na thamani ya Sh bilioni 102," alisema Mashimba.

Akizungumzia Soko la Kimataifa la Dagaa la Kasenda Chato, Waziri huyo alisema soko hilo lilijengwa mwaka 1995 na baadaye kufanyiwa maboresho mwaka 2017 kwa ufadhili wa serikali ya Japan wa takribani Sh milioni 320 na linatumiwa na wafanyabishara 167 na kuhudumia jumla ya watu 12,528 hadi 21,425.

"Soko hili linahudumia masoko ya ndani na nje ya nchi ambapo wafanyabishara kutoka nchi za Rwanda, DRC, Burundi, Uganda, Zambia na Malawi hufaidika na soko hili na pia wafanyabishara wa ndani kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Dodoma na sehemu nyingine wanakuja," alisema.

## Mvomero washauriwa

Scanned with CamScanner

Pg. 4 – 19/01/2021 – Daily News.

# Livestock stakeholders eye livestock-based industries

LIVESTOCK stakeholders eye the implement of a special five-year programme (2021-2025) to push for animal-based industries across the country.

The strategy, among other things, will incorporate market-oriented researches to ensure there are enough raw materials for all livestock-based industries. Primarily, the animal-based raw materials are hides, milk, meat and hoofs, just to mention a few.

According to Tanzania Livestock Research Institute (Taliri) Acting Director-General, Dr Jonas Kizima, preliminary studies have discovered that most industries in the livestock products category are underperforming due to poor production and supply of raw materials.

"The programme seeks to enable stakeholders in the beef and dairy cattle chain in all regions to improve their performance by adopting better technologies and practices so that they may stand a chance of feeding relevant industries," he briefed.

He informed that the envisaged programme would introduce and help livestock keepers from across the country to embrace hybrid animals, best animal health services, animal compounded and feeds, animal husbandry infrastructure, milk handling, grazing systems and good dairy animal genetics.

"For instance," he added, "most of the livestock keepers encounter the technical challenge of inbreeding, which denies their cattle to grow healthier." He added there would also campaign to impart knowledge and skills to livestock keepers.

"If all goes well, we plan to establish centres of excellence for varied livestock facets in different zones to meet raw material demand for industries in each zone," he said.

For his part, Acting Director of Livestock Institute Training Authority (Lita) Balija Luyombya said the state-owned authority was also finalising plans to start training the youth in best animal keeping practices.

He said the programme focused on different training programmes of livestock keepers from across the country.

Development includes making efforts to comply with President John Magufuli's directives to revive and promote animal-based industries in Tanzania for the coming five years.

In his remarks during the inauguration of the 12nd Parliament in Dodoma in November last year, President Magufuli said, in five years, the government would construct seven major abattoirs in different regions with the capacity to slaughter at least 6,700 cattle and 11,000 goats per day.

Scanned with CamScanner

18/01/2021 Pg. 4.

# Govt refutes reports of Nile Perch dying in Lake Victoria

By Guardian Correspondent, Mwanza

THE Government has dispelled fears from people living around Lake Victoria on reports spreading in the social media over widespread dying of the Nile Perch in the lake, saying the reports were false and should be ignored.

Refuting the reports to reporters in Mwanza at the weekend, the Livestock and Fisheries Permanent Secretary (Fisheries Division) Dr Rashid Tamatamah said reports of Nile Perch dying in great numbers in the Uganda's side of Lake Victoria were reported since early this month.

Tamatamah said after receiving the reports the ministry including its institution - Tanzanian Fisheries Research Institute (TAFIRI) based in Mwanza liaised with Lake Victoria fisheries officials on the Tanzania side including the Tanzania Fishing Union (TAFU) and after following up there was no such thing anywhere on the Tanzania's side of the lake.

The PS further said death to the Nile Perch was normally attributed by seasonal water up and down circulation in the lake and that this kind of fish live in the middle and upper waters which have enough oxygen for them.

"In our follow up on the issue we liaised with Uganda's fisheries officials who informed us that they sent samples of the dead fish to the laboratory for examination to find out whether they died by any kind of poisoning.

Uganda Fisheries Department assured us that no traces of poison were found of the dead fish examined adding that such incidents happen every year due to mixing of water, very deep water with little oxygen mixing with surface water," he added.

Tamatamah said even though such deaths of fish have not been reported in the Tanzania's side of the lake, but there was always the possibility for that to happen, hence he said, the ministry and other fisheries stakeholders were closely following up on the issue.

Scanned with CamScanner

**Takwimu>>** Watu 800 wadaiwa kufa kwa ugonjwa wa homa ya nguruwe

# Marufuku kula nyama ya nguruwe Kahama

**NA SALVATORY NTANDU,** *Kahama*

MLIPUKO wa ugonjwa wa homa ya nguruwe Wilaya ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga, umeifanya serikali mkoani humo kupiga marufuku, uuzaji, usafirishaji na ulaji wa nyama ya nguruwe.

Hatua hiyo inatokana na ugonjwa huo kudaiwa kusababisha vifo vya nguruwe zaidi ya 800.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusiana na hatua zilizochukuliwa na serikali baada ya kujitokeza kwa ugonjwa huo.

Alisema wamelazimika kuchukua hatua hiyo ili kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya ugonjwa huo ambao unaua nguruwe kwa kasi.

"Kwa sasa Kahama biashara ya wanyama aina ya nguruwe imepigwa marufuku, lengo ni kudhibiti ugonjwa huu, wataalamu wetu wanaendelea kufanya utafiti kuhakikisha wanaudhibiti mapema ili kuzuia madhara yasijitokeze zaidi," alisema Macha.

Aliwataka walaji wa nyama ya nguruwe kuacha kula nyama hiyo hadi watakapotangaziwa na serikali, badala yake watumie vitoweo vya wanyama wengine.

Mkuu wa Idara ya Mifugo wa Halmashauri ya Mji Kahama, Dk. Damin Kilyenyi, alikiri kuwepo kwa ugonjwa wa homa ya nguruwe na kusema unasababishwa na mwingiliano wa nguruwe pori na wanaofungwa nyumbani.

"Ugonjwa huu unawaathiri wanyama aina ya nguruwe tu, na hauna madhara kwa binadamu na wanyama wengine, dalili zake ni mnyama kuacha kula, kutokwa damu masikioni, kwenye macho na aishi kwa siku tatu ndio anapoteza maisha," alisema Kilyenyi.

Alibainisha kwamba mpaka sasa ugonjwa huo hauna chanjo wala dawa ambapo mnyama akipata lazima afe na kuwataka wafugaji kuchukua tahadhari.

Mfugaji wa nguruwe katika Mtaa wa Mhongolo, Evans John, alisema mpaka sasa nguruwe 17 katika banda lake wamekufa kutokana na ugonjwa huo.

"Nguruwe akipata ugonjwa huu anaanza kutetemeka, hali chakula, anatokwa damu masikioni na kwenye macho, anaaza kubadilika rangi na baada ya hapo hufa ghafla, nimepata hasara ya zaidi ya sh. milioni 2," alifafanua.

Wilaya ya Kahama inatajwa kuwa na wafugaji wengi wa wanyama hao huku idadi ya nguruwe ikitajwa kufikia 2,000.

Scanned with CamScanner